

HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz
Tovuti:www.nsimbodc.go.tz



S.L.P 688

MPANDA

Press No: NDC/ICPRU/Press no.18

25 Julai 2018

TAARIFA KWA UMMA/VYOMBO VYA HABARI.

ZIARA YA NAIBU WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) MH.JOSEPHAT KANDEGE KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Mwailwa Smith Pangani** anawataarifu Wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kuwa Leo Julai 25, 2018 Naibu waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa **Mh.Josephat Kandege** atafanya ziara katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Akiwa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mh.Kandege atatembelea Kituo cha Afya Katumba ambapo atakapokea Taarifa ya Maandalizi ya Ujenzi na Ukarabati wa Kituo hicho, pia atatembelea kituo cha Afya Kanoge kwa ajili ya Ukaguzi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kituo hicho.

Naibu Waziri Kandege pia atafanya Ukaguzi wa Ujenzi wa Jengo jipya la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Imetolewa na :

A handwritten signature in black ink, appearing to read "John A. Mganga".

John A. Mganga
Afisa Habari Mawasiliano na Uhusiano(W)
Kitengo cha Habari Mawasiliano TEHAMA na Uhusiano,
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo